

# Tunataka uwe salama!

*Kidonge Kimoja cha Fentanyl Kinaweza Kukuua*


Fentanyl kwa sasa ni ya kawaida sana kwenye jamii yetu; hii dawa ni yenye nguvu na imetengenezwa kwa opioid ambayo ni kama morphine lakini ina nguvu mara 50 mpaka 100. Fentanyl haina harufu, ladha na rangi. Vijana wanafikiri wanatumia “blues” OxyContin au Xanas, lakini watumia vidonge vilivyozunguushiwa fentanyl. Kinga bora ni kuongea na mwanafunzi wako kwamba usichukue dawa zozote ambazo hajizatoka kwa daktari. Hii inamaanisha usichukue vidonge hata kama ni kutoka kwa marafiki. Haya mazungumzo yanaweza kuokoa maisha ya mtoto wako. *Kidonge kimoja kinaweza kukuua.*

## MIKAKATI MINGINE YA KUZUIA INAJUMUISHA:

- **Mawasiliano ya Wazi:** Moja ya njia muafaka ya kuwalinda vijana katika kutegemea madawa ni kuwa na maongezi ya wazi na kuwaelimisha kwenye hatari ya kutegemea kutumia madawa. Kuwasilikiza bila kuwa hukumu ni kitu muhimu unaweza kumhakikishia kama mtu mzima anayemuamini.
- **Angalia mabadiliko ya Tabia:** Angalia mabadiliko ya tabia kama vile kula kusiko kwa kawaida au mwenendo wa kulala, kutokuwa na nguvu, dalili ya kuwa na unyongovu au wasiwasi, kukasirika kusiko kuwa kwa kawaida, kuporomoka kwa alama za masomo, kukosa hamu ya kufanya shughuli wanazo penda, na kubadilika kwa mitindo ya nguo ghafla. Amini silika yako. Kama utaona mabadiliko, uliza kuhusu mabadiliko.
- **Angalia kwenye Mitandao ya Kijamii:** Ongea na mtoto wako kuhusu matumizi yao kwenye mitandao ya jamii. Kwenye mitandao hutoa jukwaa la mazingira kwa watu wengine kuuza madawa. Madawa yanaweza kutolewa kwa mtu uliye kutana naye kwenye mitandao.

## NYENZO:

- Kata ya Marion ya Kutibu Madawa ya Kulevya  
503-588-5358  
[www.co.marion.or.us/HLT/pages/aandd.aspx](http://www.co.marion.or.us/HLT/pages/aandd.aspx)
- Kata ya Polk ya Kutibu Madawa ya Kulevya  
503-585-3012  
[www.co.polk.or.us/bh](http://www.co.polk.or.us/bh)
- Bridgeway Recovery  
503-399-5597  
[bridgewayrecovery.com](http://bridgewayrecovery.com)



*Ni vigumu kuonyesha tofauti kati ya vidonge vya kweli au vya kutengeneza. Fentanyl haina harufu, ladha na rangi.*